



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI GEITA



Kumb. Na. AB.55/451/01/50

TAREHE: 24/05/2022

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Geita anawatangazia wananchi wote nafasi za ajira ya kudumu kwa kada mbalimbali kama ilivyoainishwa katika mchanganuo ufuatao.

1.0 MTENDAJI WA MTA A DARAJA III - NAFASI KUMI (10)

1.1 MAJUKUMU YA KAZI.

- Kusimamia na kutekeleza sheria ndogo pamoja na sheria nyingine zinazotumika katika Mtaa.
- Kushauri kamati ya Mtaa kuhusu mipango ya maendeleo katika Mtaa.
- Kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria zinazotekelezwa na Halmashauri katika Mtaa.
- Kusimamia na kutekeleza mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umaskini katika Mtaa.
- Kusimamia ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote.

1.2 SIFA ZA MWOMBAJI:

- i. Mwombaji awe na Elimu kidato cha Nne (IV) au sita (VI).
- ii. Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

1.3 MSHAHARA:

Ngazi ya Mshahara ni TGS B.

2.0 DEREVA DARAJA II - NAFASI TATU (3)

2.1 MAJUKUMU YA KAZI:

- Kupeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
- Kufanya usafi wa gari.
- Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake wa kazi.

2.2 SIFA ZA MWOMBAJI:

- Awe amehitimu kidato cha Nne.
- Awe na leseni daraja E au C1
- Awe na uzoefu usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
- Awe amehitimu mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari (**Basic driving**) kutoka Chuo cha Mafunzo ya Ufundi stadi (VETA) au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
- Waombaji wenye cheti cha Majaribio ya Ufundi daraja la II watafikiriwa kwanza.
- Awe na Umri kuanzia miaka 18 hadi miaka 45.
- Awe ni raia wa Tanzania.

2.3 MSHAHARA:

Ngazi ya Mshahara ni **TGS B**.

3.0 KATIBU MUHTASI DARAJA III - NAFASI TATU (3)

3.1 MAJUKUMU YA KAZI:

- Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida
- Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anamofanyika kazi na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.

- Kusaidia kutafuta na kumpa Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
- Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake majalada, nyaraka au kituo chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini
- Kusaidia kupokea majalada, kuyarudisha sehemu zinazohusika
- Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na msimamizi wake wa kazi

3.2 SIFA ZA MWOMBAJI:

- i. Awe amehitimu Kidato cha nne na kuhudhuria Mafunzo ya U hazili na kufaulu Mtihani wa hatua ya tatu
- ii. Awe amefaulu somo la hati mkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika
- iii. Awe amepata mafunzo ya computer kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti
- iv. Awe na Umri kuanzia miaka 18 hadi miaka 45.
- v. Awe ni raia wa Tanzania.

3.3 MSHAHARA:

Ngazi ya Mshahara ni **TGS B.**

NB: Mtumishi atakayeajiriwa hataruhusiwa kuhamu kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu (3) tangu tarehe yake ya ajira.

UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI

Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **07/06/2022** saa **9:30** Alasiri. Maombi yatumwe kwa njia ya Posta kwa **S.L.P 384, Geita** au yaletwe Masjala ya Halmashauri ya Mji Geita, watakaokidhi vigezo watajulishwa kwa simu na katika mbao za matangazo ili kuweza kuja kwenye usaili.

Tangazo hili limetolewa na,

L.J. Kyangalla,

KAIMU MKURUGENZI WA MJI.

**MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
GEITA.**